



# Jifunze kuimba

...na Joett

Vocal Drills Vol. 1, 2, 3 & 4

**Mazoezi Ya  
Sauti Fasta!**

★★ POWERED BY ★★  
JoettMusic.com



**"Badili kabisa sauti yako  
ya kuimba na mazoezi  
maalum ya sauti"**

## **Jifunze Kuimba na Joett Mkito.com: Vocal Drills Volume 1**

**K**wa awamu nyingine tena, na tena safari hii kwa maboresho yalio fuata mahitaji muhimu katika kujifunza kuimba kupitia mtandao, ninawaitea toleo mpya kabisa Jifunze Kuimba na Joett Mkito Volume 1. Hili toleo ni muhimu katika kukuwezesha kuingia katika mstari wa mafunzo ambayo bila shaka, yatakuletea mafanikio ya haraka.

Kabla ya kuanza, hakikisha una download na kufanya zoezi langu la pumzi Mkito. Bila ya kuzungumza maneno mengi, nataka niwaachie toleo hili la kwanza (Vol. 1) msikilize mifano nakuendelea na mchanganyiko wa mazoezi ya sauti kwa takriban dakika 8. Mifano ipo. Nikusikiliza tu na kufuata hiyo mifano, na la msingi kabisa nikuachia sauti ifuate mkondo wake. Usilazimishe sauti. Iachie ifuate kinanda na maelekezo mwanana.

Ukiwa na maswali, jiskie huru kuniuliza, au soma nakala kadhaa nilizo andika kwenye blog langu pale [JoettMusic.com](http://JoettMusic.com) au [JoettMusic.Blogspot.com](http://JoettMusic.Blogspot.com)

## **Jifunze Kuimba na Joett Mkito.com: Vocal Drills Volume 2**

**V**olume 2 ni muendelezo wa Vol. 1. Kwa maana ni lazima ufanye Vol. 1 kabla haujafanya Vol. 2. Kwa mara nyingine tena, nita sistiza mfuate maelekezo kama yalivo kwenye toleo hili. Mazoezi haya yana dakika 7. Ukishaweza kufanya haya mazoezi, sasa utakua na mazoezi mawili. Yaani Vol. 1 & 2 katika ratiba yako ya mazoezi ya sauti ya kila siku; na utatakiwa kufanya yote kwa pamoja kufuata mlolongo huo huo wa Vol. 1 kuingia Vol. 2. Kumbuka, madhumuni ya haya mazoezi ni ku re-balance sauti yako, au kurekebisha matumizi ya sauti yako ili uweze kuimba kwa urahisi kwenda juu na kwenda chini; na mpangilio na ratiba hii ndio itaweza kukupa wewe huo uwezo kwa njia ya haraka na salama zaidi. Tafadhali usianze kukurupuka na ku-download vitu olela kwenye internet. Tafadhali fuata maelekezo yangu na mazoezi niliokuandalia ili uweze kupata mafanikio ya uhakika.

### **Jifunze Kuimba na Joett Mkito.com: Vocal Drills Volume 3**

**M**azoezi ya Vocal Drills Volume 3 ni muendelezo wa Vol. 2. Kwa mara nyingine tena, fuata maelekezo. Kama unayo maswali ama kuna kitu kinakushinda, tafadhali uliza. Nitaweza kukupa ushauri. Lakini cha msingi nikufuata maelekezo na kufanya mazoezi stahiki kama nilivowaandalia hapa.

Ukishaweza haya mazoezi ambayo muda wake ni takriban dakika 5, unatakiwa kuunganisha Vol. 1, 2 & 3 katika ratiba yako ya mazoezi ya sauti ya kila siku.

### **Jifunze Kuimba na Joett Mkito.com: Vocal Drills Volume 4**

**V**olume 4 ndio toleo la mwisho katika awamu hii mpya ya Jifunze Kuimba na Joett Mkito. Fuata maelekezo. Panapokupa taabu, tafadhali niulize nikupe muongozo. Ukishaweza hili zoezi la takriban dakika 10, sasa utakua unamazoezi ya sauti Vol. 1, 2, 3 & 4 katika ratiba yako ya kujifunza kuimba. Kwahivyo, kilamara unapo kaa kufanya mazoezi yote haya kwa pamoja, unapaswa kufanya zoezi la pumzi kabla ya Vol. 1 alafu kuendelea na mazoezi ya Vol. 2, 3 & 4 bila ya kusimama. Jumla ya muda wa mazoezi ukiunganisha hizi Volume zote 4 ni dakika 30.

Kumbuka, madhumuni ya haya mazoezi ni ku re-balance sauti yako, au kurekebisha matumizi ya sauti yako ili uweze kuimba kwa urahisi kwenda juu na kwenda chini; na mpangilio na ratiba hii ndio itaweza kukupa wewe huo uwezo kwa njia ya haraka na salama zaidi. Tafadhali usianze kukurupuka na ku-download vitu olela kwenye internet. Tafadhali fuata maelekezo yangu na mazoezi niliokuandalia ili uweze kupata mafanikio ya uhakika.

Nilicho kifanya hapa nikujaribu kuwezesha watanzania wote popote walipo, kupata mafunzo stahiki ya sauti bila ya gharama ya kuhudhuria mafunzo ya sauti darasani pamoja na mimi. Maelekezo na mazoezi haya ni nyeti kwa kukuwezesha kufikia malengo yako. Sikiliza. Tenda. Utapata faida kubwa sana kwenye swala la kuimba. Amini hilo!

## **Muongozo wa Mazoezi**

- Download mazoezi [Mkito.com](http://Mkito.com)
- Weka kwenye CD
- Tumia chombo cha muziki cha kupigia CD
- Fanya mazoezi ndani ya chumba na sio maeneo ya wazi, wala sio kwa kutumia simu yako ya mkononi na headset za masikio.

Nawatakia mafanikio mema!

# Joett

Vocal Coach